


Kusafisha Pampu yako ya Kukamua Maziwa ya Mama (Swahili)

Maelekezo ya Kuosha Seti yako ya Vifaa vya Pampu ya Kukamua Maziwa ya Mama

1. Nawa mikono yako kwa maji ya vuguvugu na sabuni.
2. Tenganisha kila kipande kwa uangalifu.
3. Vipande vinne lazima vioshwe baada ya kila kipindi cha kutumia pampu ya kukamua maziwa ya mama. Vipande hivyo vinne ni zinara ya matiti, chupa ya pampu ya kukamua maziwa ya mama, kiwambo na vali ya kudondosha matone yenye mwelekeo mmoja. Ikiwa unatumia kifaa cha kukusanya dang'a, tafadhali hakikisha kwamba kimesafishwa pia.
4. Tyubu, vifuniko na adapta ya kuunganisha tyubu kwenye pampu ya kukamua maziwa ya mama havihitaji kusafishwa.
5. Tumia beseni uliyopewa, burashi ya chupa na sabuni ya kuosha vyombo unapoosha sehemu za pampu.
6. Ruhusu seti yako ya vifaa vya pampu ya kukamua maziwa ya mama ikauke au ukaushe kwa taulo safi ya karatasi. Mifuko ya usafi inayoweza kuwekwa kwenye maikrowevu na burashi ya chupa hutumiwa kusafisha seti za vifaa vya pampu ya kukamua maziwa ya mama katika kitengo cha uangalizi makini wa watoto mahututi (Neonatal Intensive Care Unit, NICU).
7. Tafadhali osha seti yako ya vifaa vya pampu ya kukamua maziwa ya mama kwa sabuni na maji baada ya kila kipindi cha kukamua maziwa kwa pampu ya kukamua maziwa ya mama. Tafadhali weka seti yako ya vifaa vya pampu mbali na maji yanayorashika kwenye sinki ili kuhakikisha seti yako ya vifaa vya pampu ya kukamua maziwa ya mama ni safi iwezekanavyo.
8. Tafadhali nawa mikono yako tena kabla ya kuanza kukamua maziwa kwa pampu ya kukamua maziwa ya mama.



4/23

Taarifa hii haichukui nafasi ya ushauri wa kimatibabu wa mtoa huduma wako, mpango wa matibabu au elimu inayotolewa na muuguzi wako au mtoa huduma mwingine wa afya. Hakikisha unafuata mpango wako uliobinafsishwa wa huduma. Hakuna chochote katika hati hii kinachochukuliwa kuwa ushauri wa kimatibabu, utambuzi wa tatizo la afya au matibabu. Ikiwa una maswali kuhusu hii au taarifa nyingine yoyote ya kimatibabu, zungumza na mtoa huduma wako. Tafuta usaidizi kwa njia inayofaa ikiwa unahitaji huduma za matibabu za haraka. Ikiwa hauko hospitalini, piga simu kwa 911. Ikiwa wewe ni mgonjwa hospitalini, omba usaidizi kutoka kwa muuguzi wako au mhadumu mwingine kutoka kwa timu yako ya huduma.

Uliza mfanyakazi kuhusu wakalimani na huduma na usaidizi mwingine wa ufikiaji wa lugha, unaopatikana bila gharama kwa wagonjwa na familia.

